TAASISI YA ELIMU TANZANIA

MABORESHO NA MABADILIKO YA MITAALA TOKA MWAKA 1961 HADI 2010

Machi, 2013

Dibaji

Taasisi ya Elimu Tanzania ni moja kati taasisi zilizochini ya wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ikiwa na dhamana kuu ya kubuni na kuandaa mitaala ya elimu katika mfumo rasmi. Mfumo huu rasmi unahusisha shule za elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari na mafunzo ya ualimu. Kazi nyingine za taasisi kama zilivyoainishwa katika sheria iliyounda taasisi ni pamoja na kubuni na kuandaa vifaa vya kufundishia, kutoa mafunzo kwa walimu na wadau wengine na vile vile kufanya tafiti mbalimbali za kielimu.

Ili kuwe na ufundishaji katika shule au chuo zana kuu ya mwalimu ni muhtasari, hii ni kwa sababu muhtasari hutoa maelekezo ya maudhui ambayo mwalimu huyatumia darasani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji. Maudhui hayo pia yatatumika kupima kiwango cha mafanikio ya mchakato mzima wa kufundisha/kujifunza katika ngazi husika. Hii inaitwa tathmini na hutekelezwa kwa kutumia mitihani ya mwisho wa muhula na ile ya mwisho wa mwaka wa masomo. Tathmini hitimisho hufanyika mwaka wa mwisho wa ngazi ya elimu husika, hivyo kwa ngazi ya elimu ya msingi hufanyika mwisho wa miaka saba ya kukaa shuleni na kwa elimu ya sekondari ngazi ya kwanza hufanyika mwisho wa mwaka wanne wa masomo.

Maudhui yanayofundishwa katika masomo yanatokana na tafiti ambazo kitaalamu hupaswa kufanyika mara mbili katika mzunguko wa ngazi ya elimu, kwa mfano kwenye ngazi ya elimu ya msingi ambayo mzunguko wake ni miaka saba, tathmini ya kwanza ya mtaala wake itafanyika baada ya miaka mitatu na nusu, na tathmini ya pili itafanyika baada ya miaka saba. Matokeo ya tafiti hizi hupelekea kufanyika kwa kimojawapo kati ya mambo matatu, ambayo ni; ama kuendelea na mtaala kama ulivyo, kufanya marekebisho kwenye sehemu za mtaala na mwisho ni kufanya mabadiliko kwenye mtaala. Mabadiliko hufanyika inapoonekana kuwa mtaala una kasoro kubwa, wakati

ambapo marekebisho, ambayo kimsingi huhusisha mada chache katika muhtasari, hufanyika inapoonekana kuwa kuna mada zilisahauliwa, na inabidi ziongezwe, au kuna mada hazina umuhimu au zimepitwa na wakati na hivyo inabidi ziondolewe.

Andiko hili linatoa maelezo kuhusu maboresho na mabadiliko ya mitaala yaliyo wahi kutokea Tanzania tangu tupate uhuru mwaka 1961 hadi mwaka 2010. Baadhi ya maandiko yaliyotumiwa katika kuandaa andiko hili ni mihtasari iliyotumika miaka iliyopita, Mwongozo wa *Azimio la Arusha*, Ripoti ya Semina ya Wafanyakazi na Sherehe ya Miaka Kumi ya Taasisi ya Elimu (1986), taarifa ya Tume ya *Makweta,* Taarifa ya TET kuhusu Mapendekezo ya Muundo Mpya wa Masomo Katika Shule na Vyuo vya Ualimu Tanzania Bara (1991), Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, Andiko la *National Curriculum Development Framework (Unpublished), Report on Rapid survey for Reviewing Secondary Education Curriculum in Tanzania Mainland (2004),* Mitaala ya Elimu ya mwaka 2005.

Baadhi ya taasisi zilizotembelewa wakati wa kukusanya taarifa zilizowezesha kuandikwa kwa taarifa hii ni Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Maktaba Kuu ya Taifa, Maktaba ya Chuo cha Elimu Morogoro na Maktaba ya Chuo cha Elimu Korogwe. Vilevile Taasisi ilifanya mahojiano na wafanyakazi wa siku nyingi katika wizara ya elimu na wastaafu waliokuwa wanafanya kazi katika Taasisi za Elimu Tanzania.

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine katika kufanikisha matayarisho ya taarifa hii.

Dk. Leonard D. Akwilapo
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania

YALIYOMO

Dibaji 1

1.0 Utangulizi 4

2.0 Majukumu ya Taasisi ya Elimu Tanzania 4

3.0 Mabadiliko na Maboresho ya Mitaala 5

3.1 Dhana ya Mtaala 5

3.2 Uandaaji wa Mitaala 6

3.3 Mabadiliko ya Mitaala 8

3.3.1 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1967 9

3.3.2 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1979 11

3.3.3 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1997 12

3.3.4 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 2005 13

3.4 Maboresho ya Mitaala: 15

4.0 Uhusiano wa Mtaala na Muhtasari 17

5.0 Hitimisho 18

1.0 Utangulizi

Kwa muda mrefu kumekuwa na mijadala na malumbano kuhusu mitaala ya elimu nchini Tanzania. Kuna mtazamo kuwa mitaala itolewayo imekuwa inabadilishwa mara kwa mara na hivyo kwa kiasi kikubwa kuonekana kama sababu ya kushusha kwa kiwango cha elimu. Aidha wapo wanaoamini kuwa mabadiliko yanayofanywa yamekuwa yakitekelezwa bila kuwa na tafiti zinazoonesha umuhimu wa kufanyika mabadiliko hayo. Katika jitihada za kuweka kumbukumbu kwa usahihi, Taasisi ya Elimu Tanzania inatoa maelezo yenye lengo la kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza kwenye suala hili la mitaala.

Makala hii inaelezea mabadiliko na maboresho yaliyofanyika na sababu zake. Taasisi ya Elimu Tanzania ina dhamana ya kutoa mwongozo wa kitaalamu wa ufundishaji na ujifunzaji katika ngazi za Elimu ya awali, Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Vyuo vya Ualimu. Katika kipindi cha takriban miaka 52 ya taifa la Tanzania, mitaala ya elimu katika ngazi zilizotajwa imebadilishwa mara nne (4). Taarifa hii fupi itaeleza miaka ambayo mabadiliko yalifanyika na sababu zilizopelekea mabadiliko hayo.

Taarifa hii pia ina lengo la kutoa tafsiri sahihi za maneno "mtaala" na "muhtasari", maneno ambayo yamekuwa yakitumiwa na wadau wengi kwa makosa. Kuna wakati wadau wanatamka mtaala wakiwa na maana ya muhtasari, na wengine wakidhani maneno yote yana maana moja.

2.0 Majukumu ya Taasisi ya Elimu Tanzania

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) iliundwa kwa Sheria ya Bunge Na. 13 ya mwaka 1975 na kupewa mamlaka ya kuandaa mitaala pamoja na programu za kitaaluma katika ngazi za elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari na vyuo vya ualimu.

Majukumu makuu ya Taasisi ya Elimu Tanzania kama yalivyoainishwa katika sheria hiyo ni:

(i) Kubuni na kukuza mitaala kwa ngazi za Elimu Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ualimu;

(ii) Kubuni na kuandaa vifaa vya kujifunzia na kufundishia k.m. vitabu, vivunge, moduli, miongozo, vifaa vya maabara, chati za masomo,

(iii) Kutoa mafunzo ya mitaala yakiwemo mafunzo ya walimu kazini na kuwajengea uwezo wa kiutendaji watekelezaji wengine wa mitaala; k.m. Maafisa-Elimu, waratibu elimu, wakaguzi, nk.

(iv) Kufanya utafiti na kutoa ushauri kwa Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana ya elimu

Katika majukumu yote haya TET hutekeleza kazi zake kwa ushirikiano wa karibu na wizara yenye dhamana na elimu. Hii inatokana na ukweli kwamba TET ina jukumu la kuishauri serikali kwenye masuala yanayohusu utekelezaji wa mitaala ya elimu kwa ngazi za elimu ya awali, msingi na sekondari na vyuo vya ualimu. Hivyo masuala yote yanayohusu maboresho au mabadiliko ya mitaala hufanyika kwa ushirikiano wa karibu na wizara yenye dhamana na elimu

3.0 Mabadiliko na Maboresho ya Mitaala

3.1 Dhana ya Mtaala

Mtaala ni dhana pana ambayo haina maelezo ya aina moja. Wanataaluma mbalimbali wamekuwa wakitofautiana kutokana na kuwa na mitazamo tofauti ya kinadharia juu ya dhana hiyo. Kwa hiyo, kwa kifupi ni kwamba dhana ya mtaala, ikijumuisha nadharia zake na muundo wake (models) ni eneo la taaluma lenye mitazamo (perspectives) tofauti

Historia inaonesha kuwa katika miaka ya 1960 mtaala ulionekana kama mwongozo wa masomo ya kujifunzia (muhtasari wa somo), au mpangilio wa programu ya ufundishaji. Mtaala katika mtazamo wa hivi karibuni (miaka ya 1990) umekuwa na tafsiri pana na jumuishi zaidi. Maandiko mengi hutafsiri mtaala kama kioo cha jamii kinachoakisi falsafa na utamaduni wa jamii husika. Mtaala huonesha vyanzo vya maarifa, stadi na tabia anazotarajiwa kuwa nazo mlengwa, lakini vilevile mtaala utaonesha njia muafaka za kufanya tathmini, ufuatiliaji na utahini.

Katika mukhtadha wa Tanzania, mtaala ni mwongozo mpana unaoweka viwango vya utoaji elimu kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo:

(i) Ujuzi watakaoujenga wanafunzi (competences) yaani maarifa (knowledge), stadi (skills) na mwelekeo (attitudes),

(ii) Njia za kufundishia na kujifunzia zitakazotumika katika utekelezaji wa mtaala (pedagogical orientations),

(iii) Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinavyohitajika,

(iv) Upimaji, ufuatiliaji na tathmini ya mtaala husika.

(v) Sifa za kitaaluma na kitaalamu za mwalimu atakayeuwezesha mtaala husika,

(vi) Miundombinu wezeshi (enabling infrastructure) kwa utekelezaji wa mtaala wenye ufanisi,

(vii) Muda utakaotumika katika ufundishaji/utekelezaji mtaala

3.2 Uandaaji wa Mitaala

Mchakato wa kuandaa mtaala ni mrefu na endelevu, ambao huanza kwa kupitia maandiko mbalimbali ya ndani na nje ya nchi ili kupata mwelekeo wa mabadiliko ya elimu kitaifa na kimataifa. Mapendekezo na mahitaji ya elimu katika maandiko haya husaidia kuandaa zana za kuendesha tafiti kuhusu mitaala.

Tafiti huendeshwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo wazazi, wakufunzi, wahadhiri, waajiri, walimu, wakaguzi wa shule, wasimamizi wa elimu, watunga sera, wanafunzi, vyama vya kitaaluma, kitaalam na siasa, vyombo vya dini na mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali. Maoni ya wadau hutumika kutoa maamuzi ya maeneo ya mitaala (learning areas), mada, maudhui, stadi na maarifa yatakayojumuishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na vilevile kwa kuzingatia rika tofauti. Masuala mengine ya msingi yatakayoainishwa ni pamoja na taratibu za upimaji, ufuatiliaji na tathmini, na vilevile kutoa maelekezo kuhusu viwango vya rasilimali na miundombinu wezeshi vitakavyojumuishwa kwenye utekelezaji wa mitaala.

Wadau na wataalamu ambao huhusishwa katika kuandaa mitaala ni pamoja na walimu, watalaamu mahiri wakiwemo wastaafu, wahadhiri wa vyuo vikuu, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wakaguzi wa shule, paneli za masomo, taasisi na asasi mbalimbali.

Rasimu ya kwanza ya mtaala (draft) hutolewa na kujaribiwa shuleni au vyuoni ili kupata maoni, hatua ambayo hufuatiwa na uandaaji wa mitaala. Baada ya hapo, wadau hupitishwa katika mtaala ili kutoa maoni kama yapo, na kama hakuna maoni ya ziada, mtaala huidhinishwa kwa ajili ya matumizi. Mtaala rasmi huchapwa pamoja na maandiko yanayotafsiri mitaala kama vile mihtasari na miongozo mingine kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wake.

Mitaala ya elimu inayotumika Tanzania kwa wakati huu imetolewa kwa kuzingatia ngazi za elimu zilizopo, ambazo ni:

1. Mtaala wa Elimu ya Awali, (Mwaka 2005)
2. Mtaala wa Elimu ya Msingi, (Mwaka 2005)
3. Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV, (Mwaka 2005)
4. Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato V-VI, (Mwaka 2009)

5. Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti, (Mwaka 2009) na
6. Mtaala wa Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Diploma (Mwaka 2007)

3.3 Mabadiliko ya Mitaala

Chimbuko la mabadiliko ya mitaala ya Elimu ni utekelezaji wa maamuzi na malengo ya kitaifa yaliyomo katika maandiko mbalimbali yakiwemo sera, taarifa, tafiti, mapendekezo ya kitaalamu, na mipango mbalimbali ya maendeleo. Mabadiliko na maboresho ya elimu ikijumuisha mitaala ni mchakato endelevu na hayawezi kukwepeka kwa kuwa elimu inayotolewa ni lazima ijibu changamoto za jamii ambazo hubadilika na wakati.

Kwa kawaida mabadiliko ya mitaala huhusisha urekebishaji wa maeneo yote makuu ya mitaala, yaani; maudhui, upimaji na tathmini, mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Marekebisho haya yanaweza kuhusu mtaala uliokuwepo au kuunda mtaala mpya kabisa kimaudhui na mtazamo. Mabadiliko ya mitaala hushabihiana na uandishi au urekebishaji wa mihtasari yote au sehemu kubwa ya mihtasari kwa ngazi husika. Mabadiliko ya mitaala yanaweza kuhusisha baadhi tu ya ngazi za elimu au mfumo mzima.

Mabadiliko ya mitaala ni urekebishaji wa mitaala unaogusa maeneo yote makuu ya maudhui, upimaji na tathmini, mbinu na njia za kufundishia na kujifunzia na vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Marekebisho haya yanaweza kuhusu mtaala uliopo au kuandaa mtaala mpya kabisa kimaudhui na mtazamo. Mabadiliko ya mitaala husababisha uandishi au urekebishaji wa mihtasari yote au sehemu kubwa ya mihtasari kwa ngazi husika. Mabadiliko ya mitaala yanaweza kuhusisha baadhi tu ya ngazi za elimu au mfumo mzima.

Kumbukumbu zilizopo Taasisi ya Elimu Tanzania zinaonesha kuwa mabadiliko ya mitaala ya elimu nchini yamefanyika mara nne tangu tupate uhuru mwaka 1961. Aidha kumekuwa na maboresho kadhaa ya mitaala ambayo yalilenga kukidhi mahitaji mbalimbali ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kisayansi. Mabadiliko ya mitaala yalifanyika katika miaka ifuatayo:

(i) Mwaka 1967
(ii) mwaka 1979
(iii) mwaka 1997
(iv) mwaka 2005

3.3.1 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1967

Kabla ya mwaka 1967 mitaala ilikuwa ya kibaguzi na ililenga kujenga matabaka na kupata wafanyakazi wenye elimu ndogo kwa ajili ya kusaidia kazi za watawala wa kigeni.

Mabadiliko ya mwaka 1967 yalikuwa ya kwanza na yalilenga kubadili mfumo wa elimu kutoka ule wa kikoloni na kuweka wenye mtazamo wa kitanzania kwa kuzingatia elimu ya kujitegemea. Mitaala ya mwaka 1967 iliandaliwa kutokana na msukumo wa kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa hiyo mabadiliko ya mwaka 1967 yalihusu kuondoa elimu ya kibaguzi, kujenga uzalendo na kuingiza historia ya kitanzania na makabila yake, harakati za kupigania uhuru na kujenga utamaduni wa mwafrika na mtanzania. Mabadiliko haya yalilenga kuondoa mwelekeo wa elimu ya kikoloni na kujenga mfumo wa elimu ya kitanzania. Mabadiliko haya pia yalirasimisha maboresho ya mitaala ambayo yalifanyika kati ya mwaka 1961-1966 ikiwa ni pamoja na kufutwa kwa darasa la nane na shule za kati kwenye ngazi ya elimu ya msingi.

Mwelekeo ulikuwa ni kupambana na maadui watatu, ujinga, umaskini na maradhi. Dhana ya mitaala kwa wakati huo ilikuwa ni mpangilio wa masomo. Mihtasari iliandaliwa na wizara yenye dhamana ya elimu na kuchapwa na mpiga chapa wa Serikali na kusambazwa kwa wadau zikiwemo shule.

Maeneo ya kujifunza yalipangwa kwa utaratibu wa mafungu na mada kwa mfumo wa masomo. Kwa mfano: Mihutasari ya Mafunzo ya Afya katika shule za msingi zenye nyongeza maalum ihusuyo shule za vijijini, Muhtasari ya Kwata (Physical Education) darasa la I – VIII na muhtasari wa shule za msingi zenye mafunzo kwa Kiswahili. Kwa upande wa sekondari muhtasari wa "General Science" ulivunjwa na kuundwa masomo ya "Physics", "Chemistry" na "Biology".

Mabadiliko ya mwaka 1967 yaliongozwa na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea (ESR, 1967) ya kuandaa wahitimu, hususan wa elimu ya msingi kujiunga na kazi za uzalishaji. Sheria ya Elimu ya mwaka 1969 ilitolewa ili kusaidia utekelezaji wa kisheria wa Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea (EK). Mitaala iliandaliwa na kuchopekwa maudhui na vitendo vilivyoakisi Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea na iliidhinishwa na Mkurugenzi wa Elimu mwenye dhamana.

Mitaala hii ilitafsiri malengo ya Elimu ya Kujitegemea kutoka katika Kitabu cha Azimio la Arusha sehemu iliyoelezea Elimu ya Kujitegemea. Mabadiliko haya yalilenga kubadili mfumo wa elimu kutoka ule wa kikoloni na kuweka wenye mtazamo wa kujenga na kuendeleza rasilimali watu ili kuweza kusimamia na kuendeleza sekta mbalimbali za kiuchumi, kielimu, kisiasa na kiutamaduni.

Baadhi ya malengo hayo ni:

1. Kuwafunza watoto wajione kuwa sehemu ya jamii wanazoishi.
2. Elimu kupanda mbegu ya watu kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja.

3. Elimu iwafanye watoto kujiona wote ni sawa kibinadamu na kuondoa majivuno ya kikabila, rangi, dini na elimu.
4. Kujenga stadi za kudadisi na kujenga moyo wa kujiamini.
5. Kuandaa watoto kwa kazi za maisha ya vijijini na wanaojitegemea.

3.3.2 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1979

Mabadiliko ya mitaala ya mwaka 1979 yaliongozwa na falsafa ya Elimu ya Kujitegemea ili kuimarisha utekelezaji wa itikadi ya Ujamaa na Kujitegemea. Mabadiliko haya pia yalilenga kutekeleza kwa vitendo kauli mbiu za Siasa ni Kilimo na Azimio la Musoma kuhusu Elimu kwa Wote.

Mabadiliko haya yaliwezesha uanzishaji wa shule za michepuo ya Biashara, Ufundi na Kilimo. Mitaala hii ilihimiza zaidi ufundishaji unaoweka sawia nadharia na vitendo. Kupitia mitaala hii masomo ya Sayansi na Hisabati pia yaliimarishwa. Mabadiliko haya pia yalianzisha shule za sekondari za kijeshi.

Lengo la mabadiliko haya lilikuwa ni kuandaa wataalamu wa kati katika Nyanja za Kilimo, Ufundi, Biashara na Sayansikimu ili kuongeza wahitimu katika stadi hizi na kujikwamua kiuchumi.

Mabadiliko mengine yaliyotokea katika kipindi hiki yalihusu uanzishaji wa mitaala ya mafunzo ya ufundi stadi kwa wahitimu wa shule za msingi. Mabadiliko ya mwaka 1979 pia yalirasimisha maboresho kadhaa ya mitaala yaliyotokea miaka ya 1970 yakiwemo yale ya mwaka 1976.

3.3.3 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 1997

Mwaka 1982, Tume ya Rais ya Elimu iliyojulikana kama "Tume ya Makweta" ilitoa mapendekezo kuhusu uboreshaji wa mfumo wa elimu na mitaala na mapendekezo ya TET kuhusu muundo wa mitaala ya mwaka 1992 yaliyotokana na utafiti wa mwaka 1991/92 na hivyo kutoa mapendekezo ya uboreshaji wa mitaala. Kuanzishwa kwa siasa ya vyama vingi nchini pia ilikuwa mojawapo ya sababu za mabadiliko haya. Mwaka 1995, Sera ya Elimu na Mafunzo pia iliandaliwa na hivyo kutoa mwelekeo wa uboreshaji wa elimu na mitaala. Utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Tume ya Makweta na utafiti wa TET ulichukua muda mrefu kutokana na mdororo wa kiuchumi wa dunia, ukata ambao pia uliiathiri Tanzania.

Mitaala iliyoandaliwa ilitafsiri madhumuni na malengo ya ngazi mbalimbali za elimu katika shule pamoja na mafunzo ya ualimu. Mwanafunzi wa elimu ya msingi, kwa mfano, aliruhusiwa kuandikishwa akiwa na umri wa miaka 6 na uwiano wa vipindi kwa masomo mbalimbali ulibainishwa.

Mapendekezo ya muda yaliyotolewa na Tume kuhusu masomo ya darasa la kwanza na la pili yalikuwa Kusoma (22%), Kuandika (24%) na Hisabati (30%); muda uliobaki ulitumika katika michezo (6%) uchoraji (6%), uraia (3%), Afya (6%) na dini (3%). Uwiano huu ulibadilika kwa masomo ya darasa la tatu, nne, tano na sita, (Kiswahili 25%, Kiingereza 15% na Hisabati 25% ambayo ni masomo ya msingi na kuchukua asilimia 65 ya muda wa masomo (darasa 3 na 4).

Mapendekezo haya ya uwiano kwa muda kwa masomo yalihusu pia shule za sekondari ngazi ya kwanza (Kidato cha I na 4). Kwa masomo ya sekondari ngazi ya pili (Kidato cha 5 na 6) na Mafunzo ya Ualimu kwa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari yalijumuisha masomo ya kitaaluma na masomo ya Ualimu. Vitabu vya kiada na rejea pamoja na vifaa na lugha ya kufundishia pia viliainishwa katika mapendekezo ya ripoti hizi. Kiswahili kilipendekezwa kama lugha ya kufundishia kuanzia kidato cha kwanza ili

kitumike ifikapo mwaka 1985. Aidha tume ilipendekeza pia serikali ianzishe idhaa maalumu ya kutoa elimu kwa njia ya redio.

Aidha matoleo ya Sheria ya Elimu Na. 3 (1970), Na, 4 (1986), Na. 11 (1992) na Na. 10 (1995) yalitumika kuandaa mihtasari ambayo ilipitishwa na Kamishna wa Elimu baada ya kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya Elimu.

Mabadiliko haya yalipunguza wingi wa masomo kwa shule za msingi kutoka 13 hadi 7. Mabadiliko haya pia yaliwezesha uanzishaji wa somo la Maarifa ya Jamii na Stadi za Kazi kwa elimu ya msingi. Aidha masomo ya "Information and Computer Studies" kwa shule za sekondari yalianzishwa. Kubadilishwa kwa somo la Elimu ya Siasa na kuwa Civics kwa shule za sekondari ngazi ya kwanza (kidato cha I-IV) na General Studies kwa shule za sekondari ngazi ya pili (kidato cha V-VI) ilikuwa ni sehemu ya mabadiliko haya. Masuala ya sayansi na teknolojia pia yaliingizwa mfano mada za elekitroniki zilianzishwa kwa elimu ya sekondari. Mabadiliko haya pia yalihusisha uchopekaji wa masuala mtambuka katika masomo bebezi kwa ngazi zote za elimu.

Aidha mabadiliko haya yalianzisha utaratibu wa kuchagua masomo kwa mafunzo ya ualimu ngazi ya cheti (specialization) ili kujenga walimu mahiri.

3.3.4 Mabadiliko ya Mitaala ya Mwaka 2005

Mabadiliko ya mwaka 2005 yalihusu ufundishaji unaozingatia ujuzi (competence-based). Mchakato wa mabadiliko haya ulifanyika kwa vipindi tofauti kwa kila ngazi ya elimu.

Mabadiliko haya pia yaliongozwa na Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, Sera ya Elimu na Mafunzo 1995 programu za kitaifa kama vile Mkakati wa Kukuza Uchumi na

Kupunguza Umaskini, Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2025, na Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu (Education Sector Development Programme - ESDP), Uboreshaji wa mitaala ulikuwa moja kati ya malengo ya programu za kitaifa za Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) na Mkakati wa Maendeleo na Menejimenti ya Walimu (TDMS) ambazo baadhi ya malengo yake yalikuwa ni kuboresha mitaala kwa ngazi za elimu husika.

Aidha, mabadiliko haya yalikuwa ni matokeo ya tafiti zilizofanywa na TET kwa kila ngazi ya elimu na ushauri elekezi kutoka kwa wataalamu wa elimu katika maeneo ya mitaala, vitabu vya kiada na utahini. Ushauri huu ulitolewa kupitia ripoti za utafiti mbalimbali katika maeneo husika.

Harakati za mabadiliko haya zilitekelezwa kwa hatua: elimu ya awali, msingi na sekondari kidato cha I-IV mwaka 2003-2005, sekondari kidato cha V-VI mwaka 2008-2009, elimu ya ualimu ngazi ya cheti na diploma mwaka 2006-2009. Mitaala iliyoandaliwa ilihusisha kazi ya kurekebisha maudhui ya masomo yote ili kusisitiza ujuzi, dhana na kanuni za msingi. Maudhui ya Elimu ya Kujitegemea (ESR) yalichambuliwa na kujazwa katika masomo ya msingi ili kujenga na kuimarisha ujuzi unaotakiwa katika kujiendeleza kitaaluma, kujiajiri na kujiandaa na soko la ajira.

Mabadiliko haya yaliwezesha uanzishaji wa mitaala inayozingatia ujuzi yaani "Competence Based Curriculum". Masomo mapya pia yalianzishwa mfano TEHAMA, Haiba na Michezo na Kifaransa (French) kwa elimu ya msingi (Rejea Waraka Na. 2 wa mwaka 2006 kwa shule za msingi).

Mabadiliko ya mitaala yalilenga kuwa na elimu inayoendana na wakati pamoja na mabadilliko ya Sayansi na Technolojia. Mitaala ilitoa fursa ya kuwepo kwa masomo machache ya hiari (Masomo ya Kiarabu na French), kuchopeka masuala mtambuka

katika mitaala kama vile Mazingira, VVU na UKIMWI, Afya ya Uzazi na Stadi za Maisha katika masomo bebezi (carrier subjects). Maudhui ya mtaala yaliandaliwa kwa namna ambayo iliondoa ubaguzi wa jinsi na fikra mgando za jinsia na kutumia njia rafiki katika kufundisha na kujifunza.

Mabadiliko haya pia yalihusu uanzishwaji wa kozi za Ualimu wa Elimu ya Awali na Michezo katika ngazi ya cheti. Aidha masomo ya "Communication Skills", "Instructional Technology" pia yalianzishwa ili kuimarisha uwezo wa wahitimu katika stadi za mawasiliano na ufundishaji.

3.4 Maboresho ya Mitaala:

Katika aya zilizotangulia umetolewa ufafanuzi kuhusu mabadiliko mbalimbali ya mitaala kadri yalivyotokea katika miaka husika. Pamoja na mabadiliko hayo kumekuwa na maboresho mbalimbali ya mitaala ambayo yamekuwa yakitokea mara kadhaa kulingana na mahitaji ya wakati. Wadau wengi wa elimu wamekuwa wakitafsiri maboresho hayo kuwa ni sawa na mabadiliko ya mitaala. Jambo hili sio sahihi na limekuwa likileta mkanganyiko na usumbufu mkubwa kwa wadau wa elimu. Hivyo inasisitizwa kuwa katika suala la mitaala kuna wakati yanafanyika MABORESHO peke yake na kuna wakati yanayofanyika ni MABADILIKO ya mitaala.

Maboresho ni marekebisho madogo madogo yanayofanywa katika baadhi ya mihtasari ya masomo katika ngazi ya elimu. Kwa kawaida marekebisho haya hutokana na taarifa za ufuatiliaji na tathmini za utekelezaji wa mitaala hiyo. Kwa kawaida mitaala ya elimu hufanyiwa ufuatiliaji na tathmini wakati wa utekelezaji wake. Ufuatiliaji huu hufanyika muda wote wa utekelezaji wa mitaala ili kubaini upungufu uliojitokeza katika mitaala yenyewe au katika utekelezaji ambao unaweza kuathiri matokeo yanayotarajiwa.

Tathmini hufanyika aidha katikati au mwisho wa programu ili kuweza kupata vigezo vya kufanya maamuzi juu ya kuboresha, kusitisha au kubadili mtaala unaotekelezwa.

Marekebisho madogo madogo yanayotokana na ufuatiliaji au tathmini bila kubomoa (kubadili) mtaala mzima huitwa maboresho. Maboresho yanafanyika wakati wowote kama kuna sababu ya kufanya hivyo. Maboresho ya mtaala (curriculum improvement/review) hufanywa kwa lengo la kuuboresha. Maboresho hayo yanapaswa kufanywa ndani ya mzunguko mmoja au baada ya mzunguko mmoja wa mtaala (curriculum cycle) kwa ngazi husika kwa mfano miaka miwili kwa elimu ya awali, miaka saba kwa elimu ya msingi. Lengo kuu la uboreshaji wa mtaala huwa ni pamoja na kufanya masahihisho na kuingiza masuala muhimu yaliyojitokeza katika jamii kwa wakati huo.

Baadhi ya maboresho ya mitaala yaliyofanyika ni pamoja na kuanzishwa kwa somo la Sanaa na Ufundi (1976) kwa elimu ya msingi ili kutoa elimu kwa ajili ya uzalishaji mali. Aidha maboresho ya 1976 pia yalitenganisha somo la "General Science" kuwa katika masomo matatu ya "Physics", "Chemistry" na "Biology". Somo la "Mathematics" pia liliboreshwa kwa mwaka huo.

Maboresho mengine yalifanyika katika ngazi ya mafunzo ya ualimu kwa kuanzisha kozi fupi za ualimu kwa wahitimu wa shule za msingi ili kuondoa upungufu wa walimu uliojitokeza baada ya kutekeleza azimio la Elimu kwa Wote mwaka 1977/78.

Katika elimu ya msingi, maboresho ya mwaka 2006 ya kutenganisha somo la Maarifa ya Jamii na kuwa masomo matatu ya Historia, Jiografia na Uraia yalitokana na maoni ya wadau. Maboresho kama hayo pia yalifanyika katika ngazi ya sekondari mwaka 2006 ili kutenganisha somo la "Physics" na "Chemistry" kutoka kwenye somo moja lililoitwa "Chemistry with Physics". Haya yote yalikuwa ni maboresho ya mitaala ambayo yalisababisha marekebisho katika baadhi ya mihtasari (Rejea Waraka Na. 2

wa Mwaka 2006 kuhusu Marekebisho ya Mtaala wa Elimu ya Sekondari na Muundo Mpya wa Masomo katika Shule za Msingi).

4.0 Uhusiano wa Mtaala na Muhtasari

Kama ilivyoelezwa katika ufafanuzi wa dhana ya mtaala, mojawapo ya kipengele cha mtaala ni maudhui. Hii hujumuisha ujuzi, malengo na mada zitakazofundishwa. Mwongozo unaofafanua kiwango cha maudhui kwa mwanafunzi kwa kuzingatia umri, ujuzi, malengo na mada kwa kila darasa huitwa muhtasari. Jedwali lifuatalo linaonesha uhusiano uliopo kati ya mtaala na muhtasari. Itaonekana wazi kuwa wakati mtaala ni mwongozo mzima wa uendeshaji wa shule/chuo, muhtasari unalenga kutoa maelekezo ya namna ufundishaji na ujifunzaji utakavyotekelezwa ndani ya darasa. Na maelekezo hayo yanajikita katika kila somo linalofundishwa.

Mtaala	Muhtasari
1. Ni mwongozo wa mambo yote yanayohitajika katika ufundishaji na ujifunzaji kwa ngazi husika	Ni mwongozo wa maudhui ya somo litakalofundishwa kwa kila darasa husika
2. Mtaala huhusisha ngazi ya elimu mfano elimu ya msingi	Muhtasari huhusisha somo mfano hisabati kwa ngazi husika
3. Mtaala huonesha ujuzi na malengo ya jumla kwa ngazi husika	Muhtasari huonesha ujuzi na malengo mahususi kwa kila darasa
4. Mtaala huonesha sifa za vifaa na mahitaji kwa ujumla	Muhtasari huonesha mahitaji ya somo kwa kila mada au mada ndogo

5.0 Hitimisho

Dhana za maboresho na mabadiliko ya mitaala ni suala ambalo jamii inapaswa kuwa inafahamishwa na kuelimishwa kwa kina kila inapotokea. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mitaala ni mali ya jamii na hivyo kila mwanajamii ni mdau na ana haki ya kuelewa mustakabali wa mtaala na stadi zinazolengwa katika utekelezaji wa mtaala.

Andiko hili limelenga kutoa ufafanuzi wa dhana za Maboresho na Mabadiliko katika mitaala ili kuongeza ufahamu kwa wananchi katika dhana hizo mbili. Aidha, tofauti kati ya mabadiliko na maboresho ya mitaala zimebainishwa ili kutoa ufahamu mzuri kwa wadau kuhusu dhana hizi mbili. Pamoja na kufahamu tofauti zake, andiko pia limetoa ufafanuzi wa mchakato wa utayarishaji wa mitaala.

Mwisho, makala hii pia imetoa maelezo kuhusu lini mabadiliko yalitokea, sababu za mabadiliko hayo na kufafanua kuhusu kilichobadilishwa kwa kila ngazi. Maboresho ya mitaala yaliyotokea tangu uhuru pia yameelezwa ili kutoa ufahamu kwa wadau na hivyo kuwa na uelewa wa pamoja.